



Unapojuibui tafadhali taja:  
Kumb.Na.HMB/H:10/22/148

11 Desemba, 2023

Wananchi wote  
Halmashauri ya Mji,  
S.L.P 219,  
**BUNDA.**

## **YAH: TANGAZO LA NAFASI 35 ZA KAZI ZA MUDA ZA KUKUSANYA MAPATO KATIKA VYANZO VYA MAPATO HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda anapenda kuwatangazia wananchi wote nafasi za Ajira ya muda ya kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vya mapato katika Halmashauri ya Mji wa Bunda.

### **1.0. SIFA ZA MUOMBAJI**

- Awe Raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 45
- Awe Mkazi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda.
- Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- Awe mwaminifu katika kazi.

### **2.0. MAJUKUMU**

- Kukusanya na kupokea ada na ushuru katika eneo na chanzo chake alichopangiwa kwa viwango vinavyoainishwa na Sheria.
- Kuwasilisha makusanyo yote benki kwa wakati na Sheria ya fedha.
- Kutunza vitendea kazi na taarifa zinazohusu makusanyo.

### **3.0. MAOMBI YA AJIRA YAAMBATISHWE.**

- Nakala ya cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha NIDA
- Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea.
- Picha mbili za Passport za sasa (Moja ibandikwe kwenye barua ya Maombi na ya pili iambatishwe na barua ya maombi).
- Barua ya Mdhamsini pamoja na passport mbili.

### **4.0. MALIPO**

- Kiwango cha malipo kitaainishwa kwenye mkataba wako wa ajira.

## 5.0. JINSI YA KUTUMA MAOMBI.

- Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,  
Halmashauri ya Mji wa Bunda,  
288 Barabara ya Halmashauri,  
S.L.P 219,  
**31582, BUNDA, MARA.**

**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI HAYA NI TAREHE 26/12/2023 SAA 09:30 ALASIRI**

Limetolewa na:-

  
Emmanuel J. Mkongo  
**MKURUGENZI,  
HALMASHAURI YA MJI,  
TOWN DIRECTOR  
BUNDA TOWN**

**NB: Tangazo hili linapatikana pia kwenye tovuti ya Halmashauri ya Mji wa Bunda  
www.bundatc.go.tz, Instagram – bunda – town – Council na Twitter – bunda Town  
Council.**